# HISTORIA YA ROSMINIAN KWALUKONGE:

**1.0 Utangulizi**

Kama ilivyo kawaida kwa shirika la Mapendo tunaweza kufanya utume kwa njia mbili moja kwa kuombwa na jirani au kwa kuona hitaji la sehemu. Kwetu sisi kwenda Kwalukonge ilikuwa ni ombi la wanyeji wa eneo hili. Warosmini walijenga parokia ya Kristu Mchungaji Mwema Kwalukonge. Mwanzoni kabisa ilikuwa kigango cha Parokia ya Mombo kwa hiyo ilibidi Padri atoke Mombo ili kutoa huduma katika kigango hiki. Wakati mapadri wakija kutoa hudumu walikuwa mara nyingi sana wanarudi na wagonjwa ili kuwapeleka kutibiwa katika kituo cha afya Mombo. Hili lilifanyika kwa mda mrefu. Wakati hili likiendelea watu walijua fika kuwa kanisa linafanya mambo mengi na mazuri. Siku moja wakati wakimpandisha mgonjwa wakajaribu kumwomba padre ambaye aliyewasaidia siku hiyo kama shirika lingeweza kuwawekea hospitali katika eneo la Kwalukonge. Basi padre akawaambia siwezi kuwapa jibu sasa hivi ngoja nilifikishe kwa wahusi ili tuone itakuwaje. Na kweli padre huyo alilifikisha na likakubaliwa na ndiyo hapo ukaanza mchakato wa kuweza kupata ardhi kwanza. Na ifutayo ni historia fupi ya jinsi mambo yalivyoenda mpaka leo hii ninapoandika hii historia fupi ya kituo cha Afya Rosmini.

**2.0. Historia**

Mnamo tarehe 20/8/1997 maombi ya shamba lisilopungua hekta 200 yalifanywa kwa Mtendaji wa Kata (Mkalamo). Maombi yalifanywa na Fr. Stanslaus Malisa kwa niaba ya Mkuu wa Shirika.

**21/11//1997**: Kamati ya WDC Kata ya Mkalamo walika na kujadili suala la Rosmini kupewa shamba kwa ajili ya kituo cha Afya na Elimu ya Sekondari. Shirika la Mapendo lilituma wawakilishi ambao walikuwa Fr. Stanslaus Malisa na Fr. Ambrose Chuwa. Mkutano ulifanyika katika shule ya msingi Mkalamo na baada ya kujadiliana kwa kina ombi lilipitishwa.

**18/3/1998:** Barua ilitumwa kwa Mkuu wa Wilaya ya Korogwe ikiambatanishwa na muhtasari wa mkutano wa WDC uliokaa Mkalamo tarehe 21/11/1997 nakupitisha ombi la ardhi. Barua hiyo kwa Mkuu wa Wilaya inaeleza maombi ya eneo la ardhi lisilopungua hekta mia mbili (200).

**13/5/1998**: Kamati ya Ugawaji wa Ardhi ya Wilaya Korogwe ilikaa na kupokea ombi la Rosminian Fathers kuomba eneo lisilopungua hekta 200. Ilikubali na kulipeleka mkoani ambao wanauwezo wa kugawa eneo kubwa kama hilo.

**25/11/1998**; Kikao cha Kamati ya Ushauri wa Ardhi Mkoa kilifanyika Tanga mjini chini ya Mwenyekiti Mkuu wa Mkoa Capt. G. H. Mkuchika, nakupitisha maombi ya Rosminian Fathers kuomba ardhi katika Kata ya Mkalamo hekta zisizopungua mia mbili (sawa na hektari 500) katika Kata ya Mkalamo, Wilaya ya Korogwe.

**12/2/2002:** Malipo ya awali yalifanyika kwa watu wote wenye mashamba eneo hilo. Wa kwanza, Mama Grace Mfiwanga; na wengineo; Sophia Hasani, Mariam Bakari, Hatibu Bakari, Eliam Awa Aziza, Majete Abdalan Jumla ya shilingi **1,676,928** ilitolewa kama fidia kwa wenye mashamba.

**3.0. Upimaji wa ardhi (Land Survey)**

**3.0.1Mpangilio wa upimaji wa shamba**.

**3.0.2. 16/6/2002.Maafisa wa ardhi ;** kutoka kulia kwenda kushoto ni MR. MALEKO kutoka makao makuu ya ardhi Dar-es-salam, ambaye ameshikilia darubini, Mr Shao kutoka ardhi Korogwe District Tanga and Fr. Ambrose Chuwa mwakilishi wa Rosminians kutoka Lushoto

1. Jiwe la kwanza limesimikwa kutoa kusini mashariki ya barabara ya Mombo Misima



2. Jiwe la pili limesimikwa kwenye mti wa Mchocho upande wa kusini kuelekea Mto Ruvu wakiwepo wapimaji pamoja na wanakijiji cha Masimbani



3. Wapimaji wakiwa wanazugumza na Mkubwa wa shirika la Warosiminian upande wa umasaini kuelekea mto Ruvu



4. Jiwe la nne likiwekwa na wapimaji mbele ya mwenyekiti wa kitongoji cha Masimbani Mr Abdallah na mwakilishi wa kitongoji mbele ya Mkuu wa shirika Padre Polycarp Shayo



5. Jiwe la Mwisho kona kutokea Kijiji cha Makole



Wapimaji wakiwa wakihakiki upimaji wao jiwe la mwisho akiwa na Padre P. Shayo.



**4.0. Upimaji wa maji (Water Survey) Na ujenzi wa Matangi**


**10/10/2002:** – in Kwalukonge by Mr. Mgimwai – Br. Vincent Mwinami akiwa manager wa kituo. Baada ya kupimiwa shamba shirika lilianza kufanya baadhi ya vitu ambavyo viliwezekana kwa wakati huu. Mfano tulianza kulima mazao mbali mbali kama vile mahindi. Kwenye picha inaonekana vizuri watu wakiandaa mashamba kwa ajili ya kilimo





**11/12/2002:** Bomba mpya zilinunuliwa na kutandikwa kutoka mlima Mafe hadi Rosmini kituoni.

**18/1/2003**: Nyumba ya kwanza kujengwa hapa kituoni (Fathers' house na jiko). Ilijengwa na Mr. Makoye na Raphael.




**3/3/2003:** Vifaa vya ujenzi (mchanga, mawe na matofali) vililetwa kituoni kuanza ujenzi wa kituo.



**4/3/2003:**'Kontena (container) la kwanza kutoka Tanga lililetwa shambani iliyotumika kama nyumba ya Br. Vincent na store.



Baada ya hapo ilijengwa nyumba ya mabanzi ambayo ilitumika kama nyumba ya wafanyakazi na store kwa ajili ya ujenzi.



**26/3/2003:** Planning and new structure – iliandaliwa na Mr. Lusungu from Tanga municipal.

**27/4/2003**: Msingi wa Hospitali ulijengwa na Mr. Kiwia and Mushi.kutoka Lushoto















**9/5/2003**: Trustees wa Rosminians walipata kibali (Title Deed No. 17038: L.O No 171190, Farm No. 859: Block – Kwalukonge Korogwe Wilayani kwa miaka 99).

**13/10/2004:** Jiwe la msingi liliwekwa na Mkuu wa Shirika, Pd. James Flynn.







**Juni, 2007:** Usajili (registration) wa kituo cha Afya Rosmini ulifanyika.

**16/7/2007:** Kituo kilizinduliwana Mkuu wa Shirika Kanda ya Afrika Mashariki, Pd. Firmati Tarimo.

**22/1/2008:** Ombi la kufungua na kuendesha Kituo cha Afya kutoka wizarani lilitolewana Wizara ya Afya. Kumb. Na: HC 213/453/01/A/20

**22/7/2008:** Kituo kilifunguliwa rasmina Pd. Francis Quinn, Mkuu wa Shirika Mstaafu kanda ya Afrika Mashariki.

**01/07/2010**: Maabara ilisajiliwa chini ya Private Health Laboratories Board.

**6/10/2010:** Usajili (registration) ulitolewa. Namba ya kituoni 042204: - Private Health Facility.

**21/12/2010**: Kituo kilipata kibali cha kununua dawa kutoka Bohari ya dawa (MSD).

<u>WAROSMINI MKARAMBATINI.</u>

**21/7/19997** Fr.Stanslaus Malisa na Fr. Ambrose Chuwa Kufuatilia hatua za mwanzo kupata ardhi.

**Jan 2002**…Br. Vincent Mwinami alifika kwalukonge na kuanza maaandalizi ya mwanzo ya ujenzi.

**August, 2008:** Fr. Peter Bahati aliwasili kituoni.

FIRST COLU SISTERS IN ROSMINI HEALTH CENTRE

**2/3/2009:** Sr. Jenipher Raduck na Sr. Yeremiah Msangula nao pia waliwasili kituoni.

**August, 2009:**Br. Athanas Mhagama aliwasili kituoni.





**Januari, 2010:**Sr.Veronica Mushi aliwasili kituoni. Na alifariki kwa ajali ya gari mombo mwisho wa shamba tarehe 8/12/2011 jumuiya ikiwa safarini Kwamndolwa kwa jubilee ya Masisita

**23/1/2010:** Fr. Ambrose Chuwa aliwasili kituoni.



**September, 2010:** Sr.Theopista Mapunda aliwasili kituoni.

Augost. 201.Fr. Frigiel Masawe

**<u>Huduma zinazotolewa</u>**

**- 2009 June** R.C.H.ilifunguliwa katika kituo cha afya Rosmini kutoa huduma kwa mama na mtoto.

- 2009 August huduma ya VCT ( Voluntary counceling and Test.) Huduma za ushauri nasaha na kupima virusi..

- Mwaka 2010 October PM.TC.. ( Prevention of mother to child transmission) Kinga ya maambukizi ya mtoto

- 2010 Januari Huduma ya Macho kwa msimu ililetwa na madaktari Kutoka Austria.



Dr. Markusi, Andrea na Fr. Ambrosi wakimwangalia mgonjwa. …………………………



Mr. Gihard na Andrea………….



Dr. Marukusi akimpima mgonjwa

- 2010 Mai Huduma ya Kupima watoto wachanga ( DBS)

**Sola**

Tuliweza kupata sola 2008 na mwaka wa 2010 ziliongezwa zaidi kutoka panel 12 hadi 30. kutokana na mtumizi kuwa mengi pia. Kama inavyoonekana kwenye picha tulikuwa tu na panel 12 ambazo hazikutosha mahitaji ya hapa kituoni. Ndipo wafadhili wetu walipotuongezea tena panel na betri kufikia 24 ambazo zimekuwa msaada mkubwa sana katika kutupa mwanga hapa kituoni .na kwa matumizi mbalimbali kituoni.





- Mwaka 2010 Julai tulianza huduma ya ultrasound baada ya kumpata Dr. Aminiel

- Mwaka 2011 june 20th. Wakaguzi kutoka Wizara ya Afya kukagua kituo na huduma zote zinazotolewa waliridhika kwa ujumla na usafi,huduma za maabara na wahudumu waliokwepo.



Dr. Rashid DMO wa Korogwe wakiwa na wakaguzi afya toka Makao makuu



Kasoro walizoziona kituoni hatukuwa na mfamasia na Daktari (AMO) Kukosekana kwa AMO kituo kilipewa Masharti yakumpata AMO kwa muda wa miezi mitatu la sivyo kituo kitashushwa hadhi kutoka kituo cha Afya na kuwa Zahanati. Tulifanikiwa kumpata Dr. Egbert Ng'washemi mwezi wa nane na kuwa na huduma ya upasuaji mdogo kama Lampectomy, Hydroselectomy .nk.

-Mwezi wa nane 14-17 2011 madaktari na manesi wapatao kumi kutoka Austria pamoja na Dr. Mlundwa kutoka kibosho Hospital walifika kituoni kutoa huduma za macho.Watu wapatao 635 walijiandikisha kupata huduma 464 walifika kupata huduma za macho, 52 walipata operation ya macho na wote walipona vizuri na watu . 200 walipatiwa dawa na miwani.

Tarehe 24//05/2011 ombi letu la Emanuel Joseph Mlelwa kuajiriwa na serikali lipitishwa na kupangwa kufanya kazi kituo cha Afya Rosmini. Mchakato wa kuajiriwa na Serikali Sr. Jenipher Raduck na Sr. Jeremia Msangula ulikubaliwa mwezi wa June 2012. Mchakato wa kupata nyumba za wafanyakazi ulianza mwaka 2011 June tulipoomba msaada Missio Cara kujenga nyumba za wafanyakazi. Claire Dolan akiwa Project coordinator wa shirika la mapendo alituuunganisha na Ofisi za Dublin hadi tulipofanikiwa kupata fedha za kujenga nyumba 2 za familia two in one na nyumba za wafanyakazi Bachelars vyumba 8. Zilianza kujengwa April 2012 na Contractor Beda Simba na zilikamilika mwisho wa mwezi wa Saba 2012.



Zoezi la kupata maji ya kuchimba chini kituo cha Afya Rosmini na vijiji nane ulianza baada ya Mr. David Moore kutoka Canada na Claire Dolan coordinator wa project katika shirika la Mapendo walipofika Kituoni mwezi wa tano 2012 na uongozi wa Kituo wa kishirikiana na Board ya hospitali walitembelea vijiji vyote kupata taarifa kuhusu maji na. Ushiriki wa watu wote katika Huduma za RCH. Zoezi hili limekamilika June 2012.

Julay 2012 mpaka April 2013 tulikuwa na project ya kusaidia chakula kwa mama na Mtoto katika RCH yetu na ufadhili huu ulitoka Italy

Baadhi ya mambo yaliyofanyika mwaka 2013 ni uchimbaji wa bore hole ambapo maji yalipatikana umbali wa meter 120 chini ya ardhi na sehemu kubwa ilikuwa kutoboa mwamba.Mradi huu uliogarimu sh. Milion 60. Ulifathiliwa na Fr. Cristy Maclewee na Rafiki zake na baadhi ya marafiki wa Rosmini kutoka Ireland. Campuni ya Basic Intraregion kutoka Dar-essalamu ikiongozwa na Mr, Gidius ndio waliofanya hii kazi mpaka kupata maji . sehemu ya kwanza kuchimbwa meter 75 na hawakupata maji ndipo walipomchukua mtaalamu wa kupima maji kutoka chuo kikuu Dodoma ndipo alifanikiwa kupata sehemu mbili maji yanakopatikana na kuchimba sehemu moja iliyokuwa na matumaini makubwa ya maji.

**Awamu ya Pili uchimbaji wa maji ya kisima cha chini. 2013. Fr.A Chuwa and Mr.Gidius from Intraregion limited.and Rama looking at the site to drill water 1st site.**





The result in the 1st site was not good we did not get wate after 75metes.







**2nd site water after 120meters we got water 2013**



**FR.CRISTY.TESTING THE WATER AFTER THE WATER PUMP STARTING TO OPERATE**



**REA.. TECHNICHIA FIXING TRANSFORMER IN KWALUKONGE AT WATER PUMP.SITE IN 2013**



**FR.CRISTOPHER MACLEWEE.CARING BRINKS TO WATER PUMP HOUSE**



**Uchungaji Kwalukonge**

Pamoja na huduma za kijamii zilizoanzishwa mkarambatini. Chanzo cha kuelekeza huduma hiyo ni ile hudumu ya kiroho ilikuwa inatolewa kigango cha Kwalukonge kutokea parokia ya Mombo. Kigango ya Kwalukonge kiilijengwa na Pd. Antony Mitchel akiwa paroko wa Mombo na kufunguliwa na kubarikiwa mwaka 1993 na Askofu Mkude. Padri Francis Quin akiwa mkuu wa shirika wakati huo. Mwaka 2003 Padri Nazereno Natale alihamia kigango cha Kwalukonge na Kwalukonge kufanywa parokia mwaka huo. Nazareno akawa paroko wa kwanza hadi 2007 alipoondoka. Baada ya kuvamiwa na majambazi na maisha yake kuwa hatarini. Parokia iliachwa wazi kwa muda bila Padri. Mwaka 2009 – 2010 Padri Victor Mwamunyi kutumwa kufanya kazi parokiani na mwaka 2010 – 2012 .Fr Ambrose Chuwa alitumwa kufanya kazi parokiani Kwalukonge na kuhudumia Mkarambatini. Baada ya Fr. Victor Mwamunyi kuhamishwa Kwai parokiani na Fr. Peter Bahati kutoka Mkarambatini na kuhamishiwa Saruji Parokiani. Wanashirika la Mapendo wanatoa huduma za kiroho na za kijamii..

**Sala katika kituo chetu NA WAFANYAKAZI WOTE 2012**









**Pastoral activity in kwalukonge parish 2012**





**Hali ya hewa kwa ujumla**

Katika eneo hili la Kwalukonge hali ya hewa haitabiriki wakati mwingine kunakuwa na ukame mwingi kiasi kwamba watu wanakosa hata maji ya kunywa na mbaya zaidi kwa kipindi hicho hawawezi kuvuna chochote. Kwa upande mwingine watu wa eneo hili wanategemea kwa zaidi ya asilimia 80% vyakula wanavyovipata kwenye mashamba hayo. Wakati wa kiangazi maji yanakuwa ya shida sana kwa hiyo imatulazimu kujenda kisima kwa ajili ya kuhifadhia maji.



Pia wakati mvua zinaponyesha zinasababisha madhara mengi hasa zaidi kwa upande wa barabara. Wakati wa mvua ni vigumu sana kuweza kusafiri kutoka kituoni hadi Mombo kwa sababu barabara imeharibika sana na inazidi kuharibika kwa sababu inachukua pia muda mrefu kufanya matengenezo na hivyo kupelekea hali ya usafiri kuwa ngumu sana. Kwa sasa barabara ya Mombo kwalukonge ina basi moja tu linaloenda Mombo Kwalukonge ila halitoshi ukilinganisha na idadi ya watu waliopo. Na pia ni chakavu.



**UJENZI WA CHUMBA CHA UPASUAJI (Thiatre)**



**VIFAA VYA CHUMBA CHA UPASUAJI**




Ujenzi wa Thiatre ulianza 2013 na ulipata msaada kutoka Missio Austria na Life Earth group kutoka Austria Baada ya ujenzi wa Thiatre kukamilika mwaka .April.2014 tuliweza kununua baadhi ya vifaa vya thiatre kama vile operation Beds.,baada ya vitu hivyo kukamilika huduma ya operation ilianza, na pia huduma zote za operation ya macho ilifanyika kwenye hili jingo jipya .

Mwezi wa sita 2013 kituo kilipata utrsound ya kisasa kutoka Austria na pia vifaa vingine vya hospital kutokana na container iliyotumwa kutoka Ireland.

- Mwezi wa Sita 2013 tulifanikiwa kununua mashine za maabara Biochemical na Centrifige .

-Mwezi wa nane 2013 fr. Chuwa Mkurugenzi wa Kituo cha YA rosmini apipata nafasi ya kuhudhuria semina ya mwezi mmoja corrati Afika huko Nairobi course ya Usimamizi wa hospital.

Katika mwisho wa mwaka 2013.Magonjwa kumi yaliyoongoza kituon ni kama ifuatavyo

1) Malaria
2) Maambukizi ya macho
3) Uti
4) Cud
5) Pnemonia
6) Minor Surgical
7) Kuhara
8) Ari

9) PID
10) Magonjwa ya ngozi

**HUDUMA ZAMACHO**

In February 2013 Sr. Jenipher Raduck attended short course in Kibosho Hospital for 3 months sponsored by Life Earth group. When she came back she stared preparing for June Eye camp together with Dr. mlundwa from Kibosho Hospital

-In June 2013 we had eye camp in kwalukonge with Doctors from Austria..964 registered for eye camp service.. 429 attended. And 100 had their eyes operated and there was no any complications..218 people were give glass, and 90 people given medication

h 

HUDUMA YA MACHO KATIKA THIATRE MPYA JUNE 2014.



**SEMINA KUHUSU HAKI ZA MTOTO KWA WATUMISHI WA KITUO.5$^{TH}$ NOV 2014**



**HUDUMA ZA KIROHO KITUONI. NOV. 2014.BAPTISM OF ALFRED PAULO.**



**CHANGAMOTO NA MAJIRANI (wafungaji na wakulima)**



By. Fr. Ambrose UhuruChuwa .

Mkurugenzi  wa kituo cha AfyaRosmini.

Julay 2014.